**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA TAREHE 28 DESEMBA, 2021**

**WALIOHUDHURIA**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. | Joseph Elias | Afisa Uchaguzi | HWIG | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. | Joel Nkesela | Afisa Mipango | HWIG | Mjumbe |
| 3. | Bw. | Emmanuel Masaki | Afisa Mifugo na Uvuvi | HWIG | Mjumbe |
| 4. | Bw. | Leopold J.Kaswezi | Mwanasheria | HWIG | Mjumbe |
| 5. | Bibi | Dora Simbachawene | Afisa Elimu Msingi | HWIG | Mjumbe |
| 6. | Bw | Mussa L. Abdallah | Afisa Utumishi | HWIG | Mjumbe |
| 7. | Bw. | Onasis J.Mwabusila | Afisa Ugavi | HWIG | Katibu |

**SEKRETARIETI**

1. Bw. Daniel Malima
2. Bw. Baraka Kimoho
3. Bw Mohammed Mtao

**BDZ.HWIG.NA.06/01/2021/2022-KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao.Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe akawaomba wachangie hoja kwa umakini aidha alikaribishwa Mjumbe mpya Bw. Mussa Abdallah Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi aliyehamia anachukua nafasi ya Alice N.Eriyo Mkuu wa Idara ya Utumishi aliyehama. kisha akafungua kikao saa 03.34 Asubuhi.

**BDZ.HWIG.NA.06/02/2021/2022-KURIDHIA AGENDA**

Wajumbe waliridhia agenda zilizowasilishwa kwenye kikao wazijadili

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Kupitia Nyaraka za Zabuni
4. Kufunga kikao

**BDZ.HWIG.NA.06/03/2020/2021- KUPITIA NYARAKA ZA ZABUNI**

Katibu aliwasilisha barua ya maelekezo kutoka OR – TAMISEMI kuhusu utekelazaji wa miradi hii inayotekelezwa kwa fedha za Uviko – 19. Baada ya barua hiyo aliwasilisha taarifa mbele ya kikao. Wajumbe walipitia nyaraka za Zabuni ya Ujenzi wa Jengo la ICU kwa gharama ya Tshs 250,000,000.



CamScanner

Wajumbe walihoji ikiwa eneo hilo la Ujenzi lina Mgogoro, Maelezo yalitolewa kwamba eneo hilo halina Mgogoro nani eneo halali linalomilikiwa na Halmashauri. Aidha wajumbe walipitia njia za manunuzi na Kupendekeza katika ujenzi wa jengo la ICU njia ya Restricted tender itumike.

Aidha wajumbe walipitia nyaraka za Ujenzi wa Nyumba za Watumishi Itumba na Buhekela kwa gharama ya Tshs 90,000,000..00 kwa kila nyumba moja. Aidha wajumbe walipitia njia za manunuzi na kupendekeza katika Ujenzi wa nyumba za watumishi njia ya Competitive Quotation itumike.

Wajumbe walishauri kazi zote zifanyike kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na maelekezo kutoka mamlaka husika.

**BDZ.HWIG.NA.06/04/2020/2021- KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao,Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kikao kizuri kisha akakifunga kikao saa 10.52 jioni.

UMETHIBITISHWA

| | |
|---|---|
| ........................................ | ........................................ |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |
| ........................................ | ........................................ |
| **TAREHE** | **TAREHE** |

**MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA TAREHE 17 NOVEMBA, 2021**

**WALIOHUDHURIA**

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. | Joseph Elias | Afisa Uchaguzi | HWIG | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. | Joel Nkesela | Afisa Mipango | HWIG | Mjumbe |
| 3. | Bw. | Emmanuel Masaki | Afisa Mifugo na Uvuvi | HWIG | Mjumbe |
| 4. | Bw. | Leopold J.Kaswezi | Mwanasheria | HWIG | Mjumbe |
| 5. | Bibi | Dora Simbachawene | Afisa Elimu Msingi | HWIG | Mjumbe |
| 6. | Bw. | Onasis J.Mwabusila | Afisa Ugavi | HWIG | Katibu |

**SEKRETARIETI**

1. Bw. Dani Malima
2. Bw. Baraka Kimoho
3. Bi Nibwene Mwaikandage

**BDZ.HWIG.NA.05/01/2021/2022-KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao.Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe akawaomba wachangie hoja kwa umakini kisha akafungua kikao saa 10.32 jioni.

**BDZ.HWIG.NA.05/02/2021/2022-KURIDHIA AGENDA**

Wajumbe waliridhia agenda zilizowasilishwa kwenye kikao wazijadili ambazo ni:-

1. Kufungua kikao
2. Kuridhia agenda
3. Kupitisha manunuzi yafuatayo:-
    - Kuomba idhini ya ununuzi wa kazi za ujenzi kwa kutumia force Account kwa kituo cha Afya Ziba Nanga
    - Kuomba idhini ya kufanya ununuzi wa kazi ya ujenzi kwa force Account uzio wa Mnada wa Mifugo Iblogero
    - Kuomba idhini ya kufanya ununuzi wa kazi za ujenzi kwa kutumia force ACCOUNT Miradi ya Ujenzi shule za sekondari na shule za Msingi kutoka IMF
    - Kupitisha manunuzi ya huduma ya usafi na ulinzi
4. Kufunga kikao



CamScanner

**Azimio:**Wajumbe wameazimia kwamba Katibu akazifanyie marekebisho taarifa zote za manunuzi alizoziwasilisha ndipo kiitishwe kikao wajumbe waja wazijadili.

**BDZ.HWIG.NA.05/04/2020/2021- KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao,Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kikao kizuri kisha akakifunga kikao saa 10.52 jioni.

**UMETHIBITISHWA**

.............................................. **MWENYEKITI**

20/11/2021 .............................................. **TAREHE**

.............................................. **KATIBU**

20/11/2022 .............................................. **TAREHE**



CamScanner
Scanned with CamScanner

**BDZ.HWIG.NA.05/03/2020/2021- KUPITISHA MANUNUZI YAFUATAYO:-**

Katibu wa Kikao aliwasilisha taarifa ya manunuzi mbalimbali za kazi za ujenzi

i. Kuomba idhini ya ununuzi wa kazi za ujenzi kwa kutumia force Account kwa kituo cha Afya Ziba na Nanga.Katibu aliwasilisha taarifa hiyo
Wajumbe wameelekeza Afisa Ugavi akaandae taarifa ya majengo yatakayojengwa taarifa ionyeshe njia itakayotumika kufanya malipo,aidha muhtasari wa Kitengo cha Ugavi uwasilishwe uliofanyika ukieleza mapendekezo ya kitengo.

ii. Kuomba idhini ya kufanya ununuzi wa kazi ya ujenzi kwa force Account uzio wa Mnada wa Mifugo Iblogero. Katibu aliwasilisha taarifa hiyo
Wajumbe wametaka iwepo taarifa ya aina ya manunuzi ikionyesha nini kinaenda kujengwa Ibologero waione ili waweze kutoa ushauri.

iii. Kuomba idhini ya kufanya ununuzi wa kazi za ujenzi kwa kutumia force Account Miradi ya Ujenzi shule za sekondari Madarasa 92 kwa Thamani ya **Tzs.1,840,000,000.00**, Ujenzi wa Vyumba vya madarasa nane kwa thamani ya **Tshs.160,000,000.00** kwa shule za Msingi na Bweni moja la wanafunzi wenye uhitaji maalum kwa thamani ya **Tshs.80,000,000.00**. Katibu aliwasilisha taarifa hiyoWajumbe waliruhusu mchakato wa ujenzi uendelee.

iv. Kupitisha manunuzi ya huduma ya usafi na ulinzi
Taarifa iliwasilishwa na katibu wa kikao.Wajumbe waliijadili na kueleza mapungufu iliyonayo taarifa hiyo .
Taarifa hiyo iwe na Tathimini ya kazi waliyofanya
Tathimini ya vyombo vitavyotumiwa na kampuni ya usafi na ulinzi
Rasilimali watu waliopo

Wajumbe wameeleza kwamba taasisi itajiridhishaje kama walinzi wamekidhi vigezo,lazima taasisi ijiridhishe uwezo wa kampuni Silaha zitakazotumika kwenye lindo,Kampuni ina Leseni,walinzi wamefuzu mgambo,wanajua sheria za lindo na kama inamkataba wa GPSA awepo na taarifa ya tathimini ya kazi kwa kipindi kilichopita.

Kuhusu usafi kuna mapungufu yapo mfano hawatumii sabuni kudekia,hawaweki dawa kwenye choo.

Wajumbe wameelekeza Afisa Ugavi wakutane na Afisa Utumushi wafanyie kazi mapungufu hayo ili awasilishe taarifa iliyoboreshwa kwenye kikao kijacho.